# UPAKO WA MAFUTA WA MUNGU

*Watoto ni wakati wa mwisho, na kama vile mlivyosikia kwamba mpinga Kristo yuaja, hata sasa wapinga Kristo wengi wamekwisha kuwapo. Kwa sababu hiyo twajua ya kuwa ni wakati wa mwisho. Walitoka kwetu, lakini hawakuwa wakwetu. Nanyi mmepakwa mafuta na Yeye aliye Mtakatifu nanyi mnajua nyote. Sikuwaandikia ninyi kwa sababu hamwijui iliyo kweli, bali kwa sababu mwaijua, tena kwamba hapana uongo wowote utokao katika hiyo kweli. Nanyi, mafuta yale mliyoyapata kwake yanakaa ndani yenu, wala hamna haja ya mtu kuwafundisha, lakini kama mafuta yake yanayowafundisha, habari za mambo yote, tena ni kweli wala si uongo, na kama yalivyowafudisha, kaeni ndani yake (1Yohana 2:18 – 21, 27).*

Upako wa mafuta sahihi utakuwa ni nini? Kutokana na Neno la Mungu. Upendo, Amani, furaha, huo ndio upako wa mafuta. Tembea hivyo mpaka Mungu atakapoinua pazia juu na kunichukua mimi ndani, na kuifungia dunia yote inayonizunguka mimi (Wagalatia 5:22).

Sasa, Yesu alipokuja, tunaona hayo mwanzoni mwa huduma yake, kwamba baada ya Yeye kuchukua uzao wa Daudi, tukizungumzia kiroho, Roho Mtakatifu anapokuja juu yake wakati wa ubatizo wa Yohana, na akawa Masihi aliyepakwa mafuta……… sasa, kumbuka, alikuwa ni Mwana wa Mungu alipozaliwa. Alikuwa Mwana uzazi wa Mungu aliyezaliwa – kibikira. Lakini alipokuwa Masihi, ndipo pale Roho Mtakatifu alipokuja ndani yake, kwa sababu "Mesiya" inamaanisha "mpakwa mafuta" unaona? Na alikuwa mpakwa mafuta wakati Roho Mtakatifu alipokuja juu Yake (matayo 3:13 – 17, Luke 3:21 – 23). Mmenisikia nikihubiri juu ya Kondoo na hua.

Kanisa lilimchukia Yeye. Kwa nini? Alikuwa Mungu wao hasa. Walimchukia Yeye na kumkataa yeye kwamba ni Mesiya wao. Hapana, Bwana, hawakutaka Mesiya kama huyo. Na leo Kanisa linafanya jambo hilo hilo, Inakataa Neno. Hawalitaki hilo, liko



kinyume na walivyofundishwa kuamini kwa kanuni zao. Na Neno ni Mesiya (Masihi). Unaamini hilo? Vema, mwanga unaorudishwa na Neno ni nini basi? Kumuakisi Masihi, ambaye ni Roho Mtakatifu miongoni mwetu. Anarudisha nuru yake mwenyewe, akijaribu ku, popote anapoweza kupata taa kwamba angeangalia kupitia hiyo, ambayo haikushika moshi na kanuni na mambo mengineyo. Angetoa Nuru kupitia hiyo.

Kwa hiyo, hatuwezi kuwa na uhakika katika kile wengine wanachosema. Kuna kitu kimoja tu tunachoweza kuwa na uhakika nacho na hicho ni Neno. Na Neno ni Mungu.

Na Neno likipakwa mafuta linamfanya masihi, Neno lililopakwa mafuta la saa hii. Jinsi ilivyo ya kupendeza. Walilikosa hilo, Neno, Ile kweli ……. Siku zote Neno ni kweli, lakini tafsiri yao ilikuwa siyo sahihi.

Lakini wanafikiri ni kitu cha kushangaza sana duniani, kwamba wote sisi tunaweza kuunganisha mikono na kuwa mmoja. Alisema, "Yesu aliomba kwamba tuwe mmoja" hiyo ni kweli. Lakini sio mmoja wa aina hiyo.

Alisema, "kuweni mmoja kama mimi na Baba tulivyo mmoja". Ndiyo, kuweni mmoja wa aina hiyo (Yohana 17:21). Hapo sasa utakuwa ni wa namna gani? Neno na sisi itakuwa Neno lililopakwa mafuta. Huo ndio umoja wa Mungu. Unaona, Umoja wa Mungu ni Neno lililopakwa mafuta ndani yako. Unaona? Na sasa unakuwa mwana masihi wa wakati.

Sasa, angali, Musa, neno lililopakwa mafuta au hata tuiteje ….. Natumaini utaelewa, Ninaposema kwamba alikuwa ni masihi. Alikuwa Neno lililopakwa mafuta ambalo lilikuwa limeahidiwa kwa siku ile. Musa alikuwa hivyo, unaamini hilo? Hakika, neno masihi linamaanisha "Mpakwa mafuta" Unaona? Sasa. Nuhu alikuwa mpakwa mafuta wa siku yake. Ibrahim ambaye alizungumza kwamba watu wake wangechukuliwa wawe wageni utumwani miaka mia nne, na wangetolewa na mkono ulio hodari wenye nguvu na kwamba angeonyesha ishara na maajabu katika vizazi vinavyokuja, na kwamba vile ambavyo angefanya ……. Na Musa alisimama pale, lile neno

lililopakwa mafuta la siku ile. Hiyo ndiyo maana angeweka mkono wake kifuani. Kwa nini? Alikuwa amesimama uweponi pa Mungu (amen). Utukufu ule mkuu wa Shekinah ukiwa unamzunguka yeye. Kila hatua aliyoipiga ilimuwakilisha Mungu (Kutoka 3:1 – 14). Hapo ndipo Kanisa linapopaswa kusimamia sasa. Hiyo ni kweli. Badala ya hilo, tuko nje kwenye mambo ya kushangaza ya medhehebu au vitu vinginevyo.

Lakini Musa alivutiwa naye akageuka ili atazame, na pale palikuwa na ile nguzo ya Moto ikining'inia pale katika kijiti. Na hapo amesimama Musa akiwa amepakwa mafuta. Bila shaka huyu mtu hata hakujua alikuwa anafanya nini. Mifano ile aliyokuwa amepewa wakati alipokuwa amesimama na fimbo yake ya kichungaji, na alijua kwamba hiyo itakuwa ni fimbo kule jangwani, ikageuka kuwa nyoka, halafu iwe ya kufanya upatanisho, yule nyoka aliyofanya kule jangwani. Mambo yote aliyoyafanya ……… Yalikuwa ni ishara na sauti zilizozungumza na watu. Unaona, ilikuwa ni vitu fulani vilivyounganishwa naye.

Na Musa pengine hakuvitambua hivi yeye mwenye, lakini alikuwa ni Neno lililopakwa mafuta la siku ile. Alikuwa mjumbe wa saa ile, alikuwa ni masihi wa saa ile. Alikuwa mpakwa mafuta.

Sasa, yeye, Joshua na kalebu, walikuwa ni waamini wa kundi hilo (angalia) na kujaribu kuwa fundisho wengine ukweli. Lakini, angalia Shetani (Dathani na kora) waliwafanya wengine waangamie kule jangwani. Sasa, Shida ilikuwa ni nini? (Yuda 11, hesabu 16:1 – 35).

Mungu alimwita Musa. Hakutaka kwenda. Hawa manabii walikuwa na vitu vya kufanya mpaka hawaku …… Ilikuwa ni jambo gumu kulitenda. Hawakutaka kwenda kule nje na kuchekwa/kutukanwa. Walitaka wawe na ushirika, na kwenda na kundi lote lililobaki, na kwenda vizuri pamoja na ndugu. Lakini unaona, kama tu …Ninaamini …Ninasahau alikuwa ni nabii nani, alisema, "kama …….. nisipofanya hili (kwa maneno mengine), Lakini moyo wangu wote utapata moto. "Mungu amenena lazima niwaambie/niseme", kama walilipenda hilo, kama walimsulubisha yeye, kama walimpiga kwa mawe, chochote walichofanya, Mungu alizungumza moyoni mwake, na nilazima aliseme hilo, siyo kuwa tofauti, ila kuwa mtiifu. "Kutii ni bora kuliko



dhabihu, na kusikia, kuliko mafuta ya beberu" (1Sam. 15:22). Unaona, lilikuwa moyoni mwake. Lazima alifanye hilo. Ilikuwa ni uhai wake. Hangeweza kulizuia hilo. Kulikuwa na kitu fulani kilidunda dunda, ambacho kiliwasukuma wao.

Hawakuweza kulibariki hilo au kulilaani. Mungu alikuwa amewatawala mno, mpaka akawa ni sauti yake. Matendo yao. Halleluya.

Nipe mimi Kanisa ambalo limepakwa mafuta kikamilifu na Mungu mpaka matendo yao na kutembea kwao ni HII ASEMA BWANA, Ndani hasa katika utukufu wa Shekina, Nitakuonyesha Masihi (mpakwa mafuta wa Mungu) akiwa amesimama duniani.

Musa alisimama pale karibu na kijiti kila kilicho kuwa kinawaka na utukufu ule wa Shekinah. Akiwa amesimama pale, akiwa amepakwa mafuta hakujuwa hata alikuwa anafaya nini. Alikuwa tu anaitii ile sauti ilivyosema afanye. "Weka mkono wako kifuani. Utoe nje. Chukua fimbo Ikageuka kuwa nyoka. Itupe chini tena" (kutoka 4: 2 – 7).

Haijalishi mtu mwingine angalisemaje, alikuwa analifanya hilo.

"Akasema, "Bwana nionyeshe utukufu wako, na niko tayari kwenda Misri. Mimi sio msemaji vizuri, siwezi kusema vizuri. Lakini niache nione utukufu wako". Naye akamuonyesha huo. Na akaenda kule chini akionyesha mambo yale yale kwamba ni masihi aliyepakwa mafuta, mtu yule alichukuwa mavumbi ya nchi akayarusha hewani na mainzi na chawa vikatoka kwenye hilo vumbi na kuijaza nchi. Nani awezaye kuumba ila Mungu? Alichukuwa maji kutoka mtoni na akayamwaga nchi kavu, na kila tone la maji katika nchi yote ya Misri likageuka kuwa damu. Nani awezaye kufanya hayo ila Mungu? Ilikuwa ni nini? Alikuwa amejisalimisha kikamilifu kwa Neno la Mungu lililopakwa mafuta mpaka akawa ni Masihi.

Wamisri walijaribu kulikataa hilo kwa upande. Wasio amini wakalikataa. Wanaojifanya kuamini wakajaribu utaratibu wao. Lakini Neno la Mungu lilichukuwa moja kwa moja kwenye nchi ya ahadi. Hiyo ni kweli. Walipakwa mafuta. Alikuwa ni masihi.

Na Musa alipotambua kwamba aliinuliwa kwa kusudi hili na kwamba amekutana uso kwa uso na Mungu Mkuu ambaye alikuwa amemwita na kumpaka mafuta, na kumtambulisha yeye na kusema, Musa huu ni wito wako. Ninakutuma wewe. Na nitakuonyesha utukufu wangu, na niko hapa katika kijiti kinachowaka. Nenda kule chini. Nitakuwa pamoja nawe. "Hata hakuhitaji fimbo yoyote. Alikuwa na Neno, Neno lililothibitishwa. Huyo akaenda.

Iliipaka mafuta Imani aliyokuwa nayo ndani yake.
Na inatupaka mafuta sisi tuonapo kwamba sisi tunaishi katika siku za mwisho, kuona kwamba ishara hizi zote tuonazo zinatendeka, zimetabiriwa na maandiko kwamba zitatokea katika siku za mwisho. Njia yote kutoka Mbinguni mpaka kwenye nguvu za siasa, na asili ya watu, na uharibifu wa maadili miongoni mwa wanawake wa dunia, na vile ambavyo wangefanya katika siku za mwisho, na vile ambavyo wanaume wangefanya, na vile ambavyo makanisa yangefanya, vile ambavyo mataifa yangefanya na vile ambavyo Mungu angefanya. Na tunaviona vyote viko kati yetu sasa.

Oh, inaipaka mafuta Imani yetu. Inatufanya tuone mambo haya makubwa ya duara. Unaona? Inatutenganisha na mambo mengine ya dunia. Unaona? Haijalishi tu wadogo jinsi gani, tuwachache jinsi gani, tunachekwa jinsi gani, tunadhihakiwa, haifanyi tofauti yoyote hata kidogo. Yako hivyo tunayaona.

Kuna kitu fulani ndani yetu. Tumekusudiwa kimbele kuiona saa hii, hakuna kinachoweza kutzuia tusiione hiyo. Amen. Hakika. Mungu amesema hilo. Natayari limetokea tunaliona hilo, Oh, jinsi tunavyomshukuru Mungu kwa hili. Oh. Halafu inaileta Imani yako ionekane tunapoyaona haya mambo yakitokea hapa.

Ninaye rafiki mzuri kule ambaye anahubiri ujumbe huo. Ni Mpentekoste, akiwaambia watu nje kule, akijaribu kuliunganisha Kanisa pamoja, akisema inabidi tuje kwenye hili, baraza la Makanisa. Kwa nini? Baadhi wako humo ………. Kanisa la kristo ……. Mengi ya hayo madhehebu hata hayaamini kule kuzaliwa kwa bikira, na mambo haya mengine tofauti na wote wako katika hilo. Watatembeaje watu wawili pamoja ila wawe wamekubaliana? Hapo sasa, umesema 'Amen" kwa hilo, Nashangaa juu ya hili sasa. Sasa yawezakanaje mtu



aseme ni Mkristo na amejazwa na Roho Mtakatifu, na akatae kwamba lile Neno ni lile lile jana, leo na hata milele? Roho Mtakatifu ndani yako ataliitikia lile Neno, kila Neno, "Amen. Amen, Amen" Neno linaposema kitu chochote, unasema, "Hiyo ni kweli" Amen. Kwa sababu unakubaliana na Neno. Unakubaliana na Mungu. Wewe na Mungu ni mmoja. Mungu yuko ndani yako. Wewe ni Mwana wake au binti yake, inakufanya kuwa masihi wake, Lile Neno lililopakwa mafuta likiishi ndani yako.

Sasa unaona, Dathani alikuwa na wazo la kuwa wote wangeweza kufanya dini kuu kutoka hilo. Unajua, hata mtume Petro alikuwa na wazo hilo hilo pale kwenye mlima wa mageuzi. Alisema "natujenge vibanda vitatu hapa. Kimoja cha Musa na kimoja kwa Torati, na kimoja kwa Manabii, kimoja ……. (Matayo 17:1 – 8).

Na Petro alipokuwa akinena, kulikuwa na sauti iliyo shuka, ikisema, "Huyu ni Mwanangu mpendwa Msikieni Yeye". Ndipo walipotazama tena walimuona Yesu peke yake. Akiwa amesimama. Alikuwa ni Neno. Hicho ndicho upaswacho kusikiliza, ni lile Neno. Hilo ni yeye katika wakati wowote.

Angalia kile ambacho Neno linasema kwa wakati huo, na umuangalie Mungu akilipaka mafuta hilo, na kwenda nalo. Hivyo tu.

Wana wa Israeli waliifuata nguzo ya Moto kwenda nchi ya ahadi. Wale walioenda njia yote kwa hiyo walifika, wale wengine waliangamia. Angalia, Walitaka lile Neno lichanganyike na dunia. Likawafanya wakosee. Na angalia liliwafanyia nini. Lile neno …… Waliikosa hiyo kwa sababu hawangekubaliana na Neno lililopakwa mafuta. Unaona, lazima uwe na kitu cha kupinga ………… kwanza utapata kile kitu halisi ambacho mmoja atapata chakupinga kutokana na hicho. Na walikuwa nacho, na Mungu akaonyesha kuwa yeye hakuwa katika hilo.

Sasa, angalia uone, Ametutokea sisi katika umbile lile lile alilowatokea katika Agano la kale, na kwa namna ile ile Amelifanya hilo katika Agano jipya, na ameonyesha kwa Neno hilo hilo, "Kristo" yule yule inamaanisha "aliyepakwa mafuta Ni mtu tu aliyepakwa mafuta, Hivyo ndiye Kristo, aliyepakwa mafuta. Wangapi wanajua

hiyo ni kweli? Hiyo ndiyo tafsiri. Aliyepakwa mafuta, atakuwepo mtu ambaye atapakwa mafuta, atapakwa mafuta na nini? Biblia ilisema katika matendo 2 kuwa Yesu wa Nazareti, Mtu aliyethibitishwa na Mungu, amepakwa mafuta na Roho Mtakatifu, akienda huku na huko na kutenda kazi kubwa na mambo mengineyo (unaona?), Mungu huyo akidhihirishwa akithibitishwa kwamba alikuwa ndani ya mtu huyu (Matendo 2:36 na Matendo 10:38).

Na sasa, tunakuwa waliopakwa mafuta kwa Roho ile ile, masihi waliopakwa mafuta, masihi wa siku za mwisho, kuangaza huko na huku kufufuka kwa Yesu Kristo, kuonyesha kwamba Yeye siyo aliyekufa, ila yuko katika umbo la Roho Mtakatifu Akiwa ndani ya watu, akitembea kati ya Bibi Arusi wake katika Mapenzi na Yeye, akijimwaga mwenyewe ndani yake. Wanakuwa mmoja kwa ajili ya karamu ya Arusi, na ishara zile zile, zilizo ahidiwa na Mungu yule yule, katika Neno lilelile. Akifanya udhihirisho wake uleule.

Nabii wa Mungu aliulizwa: Wengine wanasema Ndugu Branham ni Mwana wa Adamu. Niliwaza ya kuwa ile nyuzo ya Moto ndiyo Mwana wa Adamu. Je nimekosea?

Hapana. Ile nguzo ya moto ni upako wa mafuta. Sasa ile nguzo ya Moto ni logosi aliyetoka kwa Mungu, ambaye hasa ni sehemu ya ukamilifu wa Mungu. Mungu alipokuwa kwenye umbo la kuweza kuonekana, ilikuwa ni ule upako wa mafuta wa Roho Mkuu aliyetoka na kadhalika, kule kujishusha kuja chini, Mungu yule logosi aliyekuwa juu ya wana Israeli, ambaye……….. alikuwa mtakatifu. Hakuweza kuvumilia dhambi. Ilipasa kuwe na toleo ladhambi pale Bustani ya Edeni. Halafu yule Logosi akafanyika mwili na kukaa miongoni kati yetu, na pale yule Logosi akakaa katika mwili wa kibinadamu, ambao ulikuwa sadaka………..

Mtu alipoumbwa kwa sura, mfano wa Mungu ……. (Mwanzo 1:26 – 27) na baadaye Mungu alikuja katika mfano /Sura ya mwanadamu ili kumkomboa mtu, hilo lilimleta mtu na Mungu pamoja. Mbingu na nchi zilikumbatiana na kubusiana pamoja. Mungu na mtu walikumbatiana pamoja kama ubaba na uwana pale Logosi alipofanyika mwili na akakaa kwetu (Yohana 1:1 – 2,14).



Yesu alisema, "Nimetoka kwa Mungu, na ninarudi kwa Mungu" je hiyo ni sawa? Baada ya kufa kwake, kuzikwa, kufufuka na kupaa, wakati mwili ulipo chukuliwa juu, kukaa katika mkono wa kuume wa Mungu ……. Sasa, simaanishi Mungu anao mkono wa kuume, Mungu ni Roho, lakini "mkono wa kuume" unamaanisha "nguvu na uwezo wa Mungu". Kwamba kwa Jina hilo kila kitu Mbinguni kinaitwa hivyo, na kinatiishwa kwa hilo. Kila kitu duniani kinaitwa kwa Jina hilo na kinatiishwa kwa jina hilo. Jina lililopita kila jina, Yesu Kristo. Sasa, huyu Logosi aliyekuwa ndani Yake, ambaye ni Roho wa Mungu, ule upako wa mafuta, kupitia utakaso wa neema ya Damu, ulileta wana kwa Mungu, ambao ni upako wa mafuta kwa Logosi huyuhuyu.

Ndugu Branham alisema, Mimi siye: Mimi ni Mtumishi wake, Na ile nguzo ya moto siyo Yeye" Ilikuwa ni katika mfano wa Roho ilikuwa ndani ya mwana wa adamu na imekuja sasa kuwapa upako wa mafuta wana wa wanadamu, ili kile kichwa na sehemu yote ya mwili viweze kuungana pamoja.

Oh, na kumbuka sasa ni yuleyule Yeye ni Yeye aliyesema katika Yohana 14:12 "Yeye aniaminiye mimi, kazi nizitendazo, naye atazifanya pia" hiyo ni sawa: Ni yeye aliyesema hivyo. Ni yeye Yesu aliyesema katika Marko 11: 24 kama ukiuambia huu mlima (siyo kama ukiuomba huu mlima) ……… kama ukiuambi huu mlima 'Ng'oka' na usione shaka moyoni mwako, lakini uamini kwamba hayo usemayo yanatukia, unaweza ukapokea kile ulichosema". Sasa kama ukisema kwa kuwazia tu, haitatokea, lakini kama kuna kitu fulani ndani yako……. Kwamba wewe ni mpakwa mafuta kwa kazi hiyo, na unajua ni mapenzi ya Mungu kufanya hivyo, na utasema hivyo, ni lazima kitokee. Ni yeye ambaye alisema hivi. Kama mkikaa ndani yangu na maneno yangu yakikaa ndani yenu, ombeni mtakacho, na mtafanyiwa". (Mt. Yohana 15:7). Oh mimi, Oh mimi unaona ninacho maanisha?

Nabii wa Mungu alishuhudia juu ya kumfufua yule kijana kule Finland: Imani iliyokuwa ndani ya moyo wangu ili kuwa imepakwa mafuta. Oh, kama tu ningeweza kulielezea hilo, Imani ambayo Mungu……..Niliyokuwa nayo kwa Mungu aliyeniambia mimi, na halijashindwa kamwe alivyoniambia, "Mazingira yalikuwa chini ya mamlaka sasa". Hapo pana jambo nililowaambia hasa miaka miwili

iliyopita, na liko hapa limekaa katika utaratibu kabisa. Jambo pekee uwezalo kufanya ni kunena Neno". Na kijana yule mdogo aliinuka kutoka kwa wafu.

Nataka kuzungumza juu ya somo la kujaribu kujenga Imani. Lazima ufanye hivyo. Kama unajenga kitu…….Kama kuna wahuduma hapa (ambapo bila shaka wapo wanajua kwamba unapokuwa unazungumza na watu unakuwa na mazingira ya kuhubiri wokovu, halafu unataka kutoa mwito kwa hilo. Na kama unataka mazingira ya uponyaji, unapata upako wa mafuta wewe mwenyewe kwa Neno la Mungu na kulitoa kwa watu, na hiyo inaliweka kundi lote katika upako wa jambo fulani, Vinginevyo, chini ya matazamio ya vitu fulani. Unaona, tunategemea kitu fulani.

Nilikuwa ninasoma historia ya Martin Luther. Na historia inasema haikuwa kitu cha ajabu kwamba Martin Luther angeweza kupinga Kanisa la Katoliki na bado akaachiliwa, ila alivyoweza kuinua kichwa chake juu ya uzushi ambao ulifuatia nyuma ya uamsho wake.

Hiyo ni sawa. Simama mwenyewe ukiwa msafi na asiye na lawama katika wito wako. Kaa na Neno la Mungu na usisogezwe na chochote. Kaa pale, dumu, katika wito wako. Kama amekupa wewe kazi kama mkulima. Lima vizuri Mungu akubariki katika hilo, na lipa fungu lako la kumi na chochote kiwacho. Matoleo yako kuifanya huduma iendelee. Kama amekufanya kuwa makanika. Na amekubariki katika hiyo kazi shikilia hiyo na umshuku kwa hiyo. Udumu mahali Mungu alipokuita.

Unaona. Kuna kitu kingine inabidi tukifahamu. Haijalishi Mungu amekubariki wewe kiasi gani. Huna haki ya kumkemea mpakwa mafuta wa Bwana, au kusema kitu chochote kinyume naye. Hiyo ni kweli. Mungu ndiye mmoja anayepaswa kulishughulikia hilo. Kama wanahitaji kemeo lolote, hao ni watoto wake. Waache peke yao. Hupaswi kufanya hivyo.

Angalia, ila hawakuipenda njia aliyoijia, ndivyo ilivyo leo. Makanisa yanawataka utaratibu wao upakwe mafuta. Mafarishayo walitaka utaratibu wao wakifarisayo upakwe mafuta, masadukayo walitaka utaratibu wao wa kisadukayo, Maherodia nakadhalika. Ndiyo ilivyo



leo. Kama wata …….. kama Mungu atatuma upako wa mafuta na awapake umoja, Oh, mimi, hawatawaambia wa uwili juu ya hilo, au wa utatu, au chochote kiwacho? Je waasemblies wataambia wa umoja juu ya hilo? "Nilikuambia tuko sahihi" Wamethodist watawaambia Wabaptist. 'Oh kijana tumempata yeye". Mnataka utaratibu wenu upakwe mafuta.

Lakini Mungu aliahidi kupaka mafuta neno lake tu. Amen. Najua hilo linachoma, lakini hiyo ni kweli. Mungu kamwe habadiliki. Anapaka mafuta neno lake. Ndiyo, Bwana. Neno la ahadi lililopakwa mafuta kwa wakati ule ndilo Mungu analolipaka mafuta. Neno lililoahidiwa la wakati ule.

Lakini ngoja niwaambie: Tunachohitaji leo ni neno la Mungu lipakwe mafuta kwa wakati huu ambalo litaleta nguvu ya Roho Mtakatifu tena.

Wafia dini wa nyakati zilizopita waliteseka vya kutisha lakini walikuwaje? Walikuwa chini ya Uvuvio, Roho wa Mungu, Nguvu. Na usisahau hili, Kanisa na ninyi mnaosikiliza kanda. Nataka ninyi mlichunguze hili. Ni kwa namna gani mtu afanye chochote nje ya nguvu za Mungu ambazo zimeachiliwa kwao?

Ninaliweka boksi hili hapa ili kuwakilisha hilo. Kama Mungu anatuma aina ya Roho miongoni mwao, hicho ndicho kitu pekee wawezacho kufanya kazi na hicho, ni Roho atendaye kazi miongoni mwao. Sasa. Vizuri tutathibitisha kwenu kwa historia ya Kanisa na kwa kufunguliwa mihuri na nguvu zile zilizoachiliwa …….. Na uone hasa Kanisa lilivyokubaliana na upako wa mafuta, na hawakuweza kufanya vinginevyo.

Sasa, Kitu cha kwanza ilikuwa ni Simba aliyenguruma. Lile Neno safi lisilochanganywa. Cha pili kule Thiatira ilikuwa ni Ndama, na ilikuwa ni mnyama wa kazi, na ilikuwa mnyama wa sadaka pia. Na je hiyo haikuwa hasa Kanisa dogo maskini la Roma ambalo lilikaa pale maika elfu ya nyakati za giza? Na kitu chochote ambacho hakikukiri Kanisa la kirumi kiliuwawa mara moja, na ilibidi wafanye kazi, watoke mahali hapa na pale.

Na ilibidi watende kazi mmoja kwa mwingine.  Tuko pale Ndama. Unaona, kile kitu kilivyoendelea, na ile sadaka ikaja na ilibidi waende. Naye alisema “usidhuru divai na mafuta”.  Walifanya nini?  Kwa kupenda kwao walienda pale na kufa.
Hawakujali kwa sababu Roho ya Kanisa katika siku ile ilikuwa ni sadaka.  Kazi, Na walitembea kwa uhuru kadiri walivyoweza, wakiwa wamepakwa mafuta na roho wa kweli wa Mungu wa wakati ule, na kuja kama mashujaa wa sadaka, maelfu kwa melfu, sitini na nane millioni waliowekwa kwenye rekodi.  Ndama, sadaka.  Oh, mimi, mnalewa hilo?



Sasa. Ni nini?  Kristo akija katika mwili wake.  Kristo ni Neno wote tunajua ule upako wa mafuta ni Kristo, ambao unakuja kwenye Neno na kulifanya Neno liishi.  Sasa, Neno liko moyoni mwako.  Unaamini uponyaji wakiungu na vinginevyo vyote.
Na Kristo, ule upako wa mafuta, unakuja katika mwili wake (Unaona muungoniko pale?, Kama vile mwanaume na mwanamke wanavyokuwa mmoja.  Sasa, Kanisa inabidi liingie kwenye huduma mpaka Kanisa na Kristo vimekuwa mmoja.  Anaweza akakupaka mafuta wewe kwa kila baraka ya Biblia.  Kila moja ni yako.  Kila kitu kilichoahidiwa cha wakati huu ni chako.  Lakini kama tukiacha kitu chochote nje sasa …….. Kama upako wa mafuta ukigusa hilo – itaupaka mafuta huo.

**Nukuu za Kiingereza**
Kwa nini watu wanayumba huku na huku Aya 34/ kumiliki malango ya Adui Aya 79 Lile shitaka  uk 30 Unasema huyu ni nani? Aya 83 – 85, 121 – 127, 138, 147 – 149/ Kwa nini unalia? Nena! Uk. 19+48 Imani kamalifu Aya 154 – 155/ Maswali na majibu  (64 – 0823E), COD uk 1019 – 1021/ kung’ang’ania (62 – 0218) Aya 12/ “Ushawishi” (64 – 0315), Aya E30 – E31/ Dunia inamomonyoka tena vipande vipande Aya 134 – 136/ Muhuri wa tano uk. 351 – 353/ Kitendawili (64 – 0418B) Aya E8.

---

Jiwe la kiroho la kujengea na. 116 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa hii, iliyokusanywa na Gerd Rodewald Friedenstr. 69 D-75328 Schomberg, Germany Simu (+49) 72357613 Fax: (+49) 72353306

---

Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itazunguka dunia. Na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyochaguliwa kimbele imesikia.
(Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724)

*Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili Andika kwa:*
*Charles E. Y. Kanju,*
*Box 553 Korogwe -  Tanga*
*E-mail: Chaelika@livel.com*
*Cellphone: 0784 704299/ 0718230098*